# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

# VIPAUMBELE VITANO VYA FURSA ZA UWEKEZAJI, 2018



## I. KILIMO

Kilimo ni uti wa mgongo Katika wilaya ya Kilwa ambapo zaid ya 80% ya wananchi wanajihusisha na shughuli mbalimbali za Kilimo ambapo takribani hekta 47,223 zinatumika kwa kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara. Mazao yanayolimwa kwa wingi katika wilaya ya Kilwa ni kama yafuatayo; kilimo cha muhogo, kilimo cha mtama, mbaazi, ufuta, viazi vitamu, kilimo cha machungwa, maembe, Nazi, kilimo cha Mwani, mbogamboga na mahindi.

Licha ya kuwa na maeneo mazuri ya kufanya shuguli za kilimo maeneo mengi ambayo yanarutuba hayatumiki ipasavyo kuweza kuleta tija katika sekta ya kilimo. Hali hii inatokana na wakulima wengi wamekuwa wakitumia nyenzoo duni za kilimo, ukosefu wa soko la uhakika wa mazao umepelekea wakulima kutokuwa na ari ya kufanya kilimo kama sekta muhimu ya kuwakwamua katika wimbi la umaskini, upungufu wa wataalamu katika sekta ya kilimo, ukosefu wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, ukosefu wa mitaji kwa wakulima na ukame.

Kwa kupitia changamoto zinazoikabiri sekta ya Kilimo Wilaya inawakaribisha wawekezaji kuja na kuwekeza katika maeneo yafuatayo katika sekta ya kilimo ili kuleta tija katika sekta ya Kilimo kwakuwa mazingira yaliyopo yanaruhusu:

A. Kuwekeza katika kilimo cha mbogamboga, matunda, matikiti, viazi vitamu, maembe, machungwa.

B. Viwanda vya kuchakata mafuta ya alizeti, nazi na ufuta

C. Viwanda vya kutengeneza bidhaa za mazao ya kilimo kama bidhaa zinazotokana na zao la muhogo, viazi vitamu, mahindi, matunda ya maembe na machungwa, mbaazi.

D. Kiwanda cha kutengeneza bia kutokana na zao la Mtama

E. Kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ambapo kuna hekta zipatazo **10,322** ambazo hazijaanza kutumika kwaajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya Mavuji, Makangaga, Matandu.

## II. UTALII

Kilwa ina maeneo mazuri ya kitalii yenye ikolojia nzuri, makumbusho pamoja na maeneo ya wanyama wa mwituni. Maeneo haya yamekuwepo kwa takribani miaka mingi iliyopita lakini hayajaendelezwa vizuri kwa kuboresha miundombinu ya kuweza kuwavutia watalii wandani na watalii wa nje. Katika wilaya ya kilwa kuna maeneo ya fuatayo ambayo ni muhimu kwa shughuli za kitalii ambayo yanavivutio vya asili, Magofu ya kale yaliyopo Kilwa kisiwani na kilwa kivinje, mapango ya Nandete yaliyopo katika kata ya Kipatimu, makaburi ya watu wakale hasa kipindi cha biashara ya utumwa yaliyopo Kilwa Kisiwani.

Vivutio vingine ni viboko waliopo mto Nyange, Misitu ya asili ambayo ina ndege wazuri na wakuvutia na fukwe nzuri zilizopo mwambao wa bahari ya Hindi.
Hivyo uwepo wa vivutio hivi unafanya kuwepo kwa hekta **844.24** ambazo zinaweza tumika kwa fursa za uwekezaji katika maeneo yafuatayo; hotel za kitalii, nyumba za kulala wageni wanotembelea vivutio vya kitalii, maeneo ya michezo kama mabwawa ya kuogelea na sehemu za kucheza watoto, kuwekeza katika usafiri wa maji kwakutumia boti ziendazo kasi.

## III. VIWANDA.

Wilaya ya kilwa ina takribani hekata **14,212** ambazo zipo kwaajili ya kufanya uwekezaji wa viwanda vikubwa na viwanda vya kati. Kuna viwanda vidogo vidogo vinavyo zalisha bidhaa hasa samani za majumbani ambazo hutengenezwa kwa ujuzi mdogo na kwa teknolojia duni, pia kuna viwanda vidogo vya kukausha samaki ambavyo vipo eneo la Kivinje na Somanga, viwanda vidogo vya kutengeneza na kufunga chumvi ambavyo vipo katika maeneo ya mashamba ya chumvi yaliyopo Kilwa Masoko na maeneo ya Kata ya Tingi, Miteja na Somanga.

Hivyo Halmashari ya Wilaya ya Kilwa inawakaribisha wawekezaji kuja na kuwekeza katika Viwanda vya kati na vikubwa kwakuwa miundombinu iliyopo inaruhusu hasa upatikanaji wa umeme wa uhakika, barabara na rasilimali watu ambavyo ni muhimu katika uwekezaji wa viwanda, uwepo wa malighafi hasa za gasi ambayo ni muhimu

kwa kutengeneza saruji, uwepo wa maji ya chumvi, uwepo wa madini ya Nitrous(vilipuzi), uwepo wa Samaki wengi na Dagaa wanaopatikana katika Bahari ya Hindi.

**Wawekezaji wanakaribishwa kuja na kuwekeza katika Sekta ya Viwanda katika maeneo yafuatayo;**

A. Viwanda vya Saruji
B. Kiwanda cha kuchimba na kuchakata Gesi
C. Viwanda vya kutengeneza vilipuzi
D. Viwanda vya kutengeneza na kufunga Chumvi
E. Viwanda vya Kuchakata Samaki
F. Kiwanda cha Mbolea

## IV. UCHIMBAJI WA MADINI NA GESI.

Madini ni sekta nyingine ya kiuchumi ambayo ni muhimu katika ujenzi wa uchumi, lakini haijawa na tija sana kwa uchumi wa wilaya ya Kilwa kwasababu hakuna wawekezaji wa kutosha kuweza kuwekeza katika uchimbaji wa madini, uchimbaji uliopo katika maeneo machache ni wa kiwango kidogo kwa kuwa wanaojihusisha katika shughuli hii ni wachimbaji wadogo ambao hawana nyenzo za kuweza kuifanya sekta ya madini iwe na tija katika Wilaya ya Kilwa.

Wilaya ya kilwa ina Maeneo ambayo madini yamekuwa yakipatikana ambayo ni madini ya gasi Maeneo ya Makangaga, Mbwemkuru na Kiranjeranje, uwepo wa mafuta na gesi katika eneo la kijiji cha Kiswele na Rushungi mwambao mwa Bahari ya Hindi na baadhi ya Maeneo katika kijiji cha Songosongo.

Hivyo Wilaya ya Kilwa inawakaribisha wawekezaji kuja na kuwekeza katika **hekta 300** za uchimbaji wa madini ili kuleta ushindani na ufanisi katika sekta ya madini na gesi ili kukuza uchumi wa Wilaya na Taifa kwa ujumla.

## V. UVUVI.

Wilaya ya Kilwa ina takribani eneo lenye maji lenye ukubwa wa wa hekta **1,221.52** linalotumika kwa uvuvi, eneo hili linatumika na wavuvi wadogo wadogo ambao wanavua kwa kutumia nyenzo duni ambazo hazileti ufanisi katika kuimalisha sekta uvuvi. Sekta ya uvuvi ni ya muhimu kwa kuwa takribani 8% ya wananchi wanajihusisha na uvuvi wa samaki.

Aidha Halmashauri ya Wilaya Kilwa inawakaribisha wawekezaji kuja na kuwekeza katika sekta ya uvuvi ili kuleta chachu ya maendeleo ya wilaya na taifa kwa ujumla.

**Wawekezaji wanakaribishwa kuja na kuwekeza katika sekta ya uvuvi katika maeneo yafuatayo;**

A. Kuwekeza katika utengenezaji wa nyenzo za kisasa za uvuvi.
B. Kuboresha miundombinu ya kuhifadhia samaki.
C. Kuwekeza katika viwanda vya kusindika samaki.
D. Kutengeneza bidhaa zinazotokana na mazao ya bahari.
E. Kuanzisha mashamba ya kufuga samaki.
F. Kuwekeza katika usafiri wa maji ili kufika katika bahari ya kina kirefu.
G. Kuwekeza katika utengenezaji wa mapambo yanayo tokana na mazao ya bahari.

IMEANDALIWA NA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W) IDARA YA MIPANGO TAKWIMU NA UFUATILIAJI © 2018